

Review Article

Dosari za Kimofosintaksia Zinazofanywa na Wajifunzaji wa Kiswahili katika Shule za Sekondari Nchini Uganda

Anifah Atuhaire^{1*}, Dkt. Adventina Buberwa²

¹(Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu) Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

²(Mhadhiri Mwandamizi) Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Article History

Received: 16.04.2025

Accepted: 22.05.2025

Published: 31.05.2025

Journal homepage:

<https://www.easpublisher.com>

Quick Response Code



Abstract: Wajifunzaji wa lugha ya pili hufanya dosari mbalimbali za kiisimu katika ujifunzaji wao. Tafiti mbalimbali kuhusu suala hili zinaonesha kuwa dosari katika ujifunzaji wa lugha ya pili au lugha ya kigeni hutokeea kama athari za lugha za kwanza za wajifunzaji. Mwandishi wa makala haya alikisia kuwa dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili hazitokani na athari za lugha za kwanza pekee, bali kuna masuala mengine yanayowasababishia wajifunzaji kufanya dosari katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Hali hii ndiyo iliyochochea raghba ya kufanyika kwa utafiti huu unaohusu dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda. Makala haya ni sehemu ya tasnifu ya uzamivu ya mwandishi wa makala. Data ya utafiti uliozaa makakala haya ilikusanywa kwa kutumia uchambuzi matini pamoja na ushuhudiaji. Uchanganuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Dosari iliyoasisiwa na Corder (1967). Matokeo ya uchambuzi wa data yamebainisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali za kimofosintaksia. Dosari hizo ni pamoja na matumizi yasiyo sahihi ya vipatanishi vya kisarufi, matumizi yasiyo sahihi ya viambishi, vielezi, virejeshi, vivumishi, kuchanganya njeo, utohozi usiofaa pamoja na kutokukanusha kwa usahihi.

Keywords: Dosari, Mofosintaksia, Dosari Za Kimofosintaksia, Wajifunzaji, Lugha Ya Pili, Lugha Ya Kigeni, Usasanyuzi Dosari.

Copyright © 2025 The Author(s): This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution 4.0 International License (CC BY-NC 4.0) which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

1.0 UTANGULIZI

Kwa muda mrefu, lugha ya Kiswahili nchini Uganda imekuwa ikifundishwa katika shule za sekondari kama somo la hiari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Mnamo mwaka 2021, serikali nchini Uganda ilipitisha ufundishaji wa Kiswahili kama somo la lazima kuanzia kidato cha kwanza hadi cha pili baada ya kuanzisha mtaala unaozingatia umilisi. Hata hivyo, kabla ya serikali kuchukua hatua hiyo, yalikuwapo baadhi ya maeneo nchini Uganda kama vile eneo la Ankole ambayo yamekuwa yakifundisha Kiswahili kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita, na bado wajifunzaji katika maeneo hayo wanaendelea kufanya dosari mbalimbali za kiisimu katika ujifunzaji wao. Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu dosari katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili (kuanzia sasa L2). Mathalani, utafiti wa Mutungu (2001), Mukuthuria (2004), Rapando (2005), Ontier (2015), Chepkwony (2011), Kisakwah (2014), Obara (2014), Gawasike (2016), Nyagah (2016), Vincent (2019), Masereka (2021) na Rutagwerera (2022). Matokeo ya tafiti hizi yanadhihirisha kuwa dosari zinazofanywa na wajifunzaji

wa Kiswahili hutokeea kutokana na athari za lugha za kwanza za wajifunzaji. Watafiti hao wamejikita sana katika kuangazia lugha ya kwanza (kwanzia sasa L1) ya mjifunzaji kama chanzo cha dosari anazozifanya katika ujifunzaji wa Kiswahili. Mathalani, Masereka (2021) alichunguza kuhusu athari za kimofosintaksia za lugha ya Kikondo katika ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa L2 katika shule za sekondari nchini Uganda. Utafiti wake uliwalenga wajifunzaji amba ni wazungumzaji wa Kikondo kama lugha yao ya kwanza katika eneo la Bwera, wilayani Kasese. Matokeo ya utafiti wa Masereka (2021) yalibaini kuwepo kwa athari za kimofosintaksia za Kikondo katika ujifunzaji wa Kiswahili mionganoni mwa wajifunzaji katika eneo hilo. Naye Mulei (2023) alifanya utafiti kuhusu mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia wa ngeli nomino za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Katika utafiti wake, anaonesha ukuruba uliopo kati ya baadhi ya nomino za Kiswahili na Luganda. Matokeo ya utafiti wa Mulei (2023) yanadhihirisha kuwa wajifunzaji amba lugha yao ya kwanza ni Luganda huhamisha kanuni za Luganda katika ujifunzaji wa Kiswahili. Tafiti hizo

*Corresponding Author: Anifah Atuhaire

(Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu) Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

zilijikita katika uchanganuzi linganishi wa vipengele veya lugha lengwa na L1 ya wajifunzaji ili kubainisha namna L1 ya wajifunzaji ilivyoathiri ujifunzaji wa L2 (Kiswahili).

Tofauti na tafiti hizo, mwandishi wa makala haya aliongozwa na mawazo ya Corder (1967) kuwa, dosari katika ujifunzaji lugha hutokana na wajifunzaji wenye we kukosea kanuni za lugha lengwa kutokana na ukosefu wa maarifa kuhusu namna ya kutumia kanuni hizo. Kwa hiyo, makala haya yana lengo moja, ambalo ni kubainisha dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda.

2.0 METHODOLOJIA

Data za utafiti uliozaa makala haya zilikusanywa kutoka uwandani kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini pamoja na ushuhudiaji. Matini zilizochanganuliwa zilihusisha kazi andishi na simulizi za wajifunzaji. Wajifunzaji walipewa zoezi la insha yenye urefu usiozidi maneno 300 juu ya kisa ambacho wasingekisahau. Uteuzi wa mbinu hii uliongozwa na mawazo ya Weigle (1999), Leijten na Van Waes (2013) ambao wanashauri kwamba katika kuchunguza dosari, wajifunzaji wapewe zoezi la kuandika insha yenye kiwango fulani cha maneno kinachopimika ili waweze kujieleza vizuri. Kwa kuzingatia maoni hayo, insha (20) zilikusanywa, (4) kutoka kwa kila kidato. Mbinu hii ilisidia kupata matini zilizochambuliwa ili kubainisha dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji.

Kwa mujibu wa Cohen na wenzake (2000), ili kuchunguza tabia changamani za wanadamu, ni lazima kutumia mbinu za ukusanyaji wa data zaidi ya moja. Kwa hivyo, mtafiti hakuwa na budi kutumia mbinu nyingine ya ukusanyaji data ambayo ingemsaidia kupata data toshelevu kuhusu dosari zilizofanywa na wajifunzaji lengwa. Ni kutokana na hali hiyo ambapo mtafiti pia aliamua kutumia mbinu ya ushuhudiaji. Aliomba kushiriki katika vipindi veya wajifunzaji darasani ili kujionea jinsi ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ulivyojukwa. Mtafiti alihudhuria kipindi kimoja kwa kila kidato katika kila shule. Kushiriki kwa mtafiti darasani kulimsaidia kushuhudia jinsi mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani ulivyojukwa. Mtafiti alipokuwa akishiriki katika vipindi darasani alikuwa akirekodi masimulizi na majibu ya wajifunzaji darasani kuhusu somo. Baadaye, mtafiti alisikiliza rekodi hizo na kunukuu sehemu muhimu, ambazo hatimaye zilichanganuliwa kwa lengo la kubaini dosari za kimofosintaksia zilizofanywa na wajifunzaji hao.

3.0 Kiunzi cha Nadharia

Uchunguzi huu uliongozwa na Nadharia ya Usasanyuzi Dosari (kuanzia sasa NUD) ambayo iliasisiwa na Corder (1967). Nadharia hii inajihuisha na uchunguzi wa utendaji wa mjifunzaji kutokana na mchakato wa kiakili wa kutekeleza kile anachojifunza katika lugha ya pili. Nadharia hii inachunguza dosari na

visababishi veya dosari hizo. Kwa mujibu wa NUD, dosari nyingi za watumiaji wa lugha ya pili zinatokana na wajifunzaji wenye we kukosea kanuni za Lg2 katika ujifunzaji wao. Kwa kuzingatia mawazo makuu haya, mtafiti alilenga kubainisha dosari za kimofosintaksia ili kubaini kama dosari hizo zilitokana na wajifunzaji wenye we kuvunja kanuni za lugha ya pili au la.

Kwa mujibu wa Corder (1967), usasanyuzi dosari unajihuisha na misingi mikuu mitano ambayo ni: kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha, kubainisha dosari, kueleza dosari, kufafanua chanzo cha dosari, na kutathmini dosari. Mwandishi wa makala haya alizingatia msingi wa kwanza hadi wa tatu kubainisha na kueleza dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji lengwa kama ifuatavyo:

- i. **Kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha:** Mtafiti alikusanya sampuli za kazi za wajifunzaji kutoka kidato cha pili hadi cha sita kwa kutumia mbinu ya uandishi wa insha na ushuhudiaji. Kwa kutumia mbinu ya uandishi wa insha, wajifunzaji walipewa zoezi la kuandika insha kuhusu siku ambayo hawangeisahau daima. Aidha, kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, mtafiti alihudhuria vipindi veya Kiswahili darasani na kurekodi matini simulizi kutokana na mafundisho ya darasani.
- ii. **Kutambua dosari:** Insha za wajifunzaji zilisomwa na kusahihishwa ili kubainisha dosari za kimofosintaksia zilizofanywa na wajifunzaji. Aidha, data ili yorekodiwa ilisikilizwa kwa umakini na kunukuliwa tungo zilizokuwa na dosari.
- iii. **Kueleza dosari:** Dosari zilizobainishwa ziliaishwa kwa kuzingatia kigezo cha kimaudhui. Dosari zilizofanana kutokana na mbinu zote mbili ziliwekwa katika kundi/aina moja na kutolewa maelezo kwa ujumla ili kujiepusha na urudiaji wa hoja kulingana na jinsi zilivyojitekeza kwenye tungo husika.

Kwa hivyo, kwa kuongozwa na NUD matokeo ya uchambuzi wa data ni kama yanavyofafanuliwa katika sehemu ifuatayo:

4.0 Dosari za Kimofosintaksia Zinazofanywa na Wajifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili katika Shule za Sekondari Nchini Uganda

Kutokana na data za utafiti zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya uandishi wa insha na ushuhudiaji, ilibainika kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali katika ujifunzaji wao. Matokeo ya uchambuzi wa data, yamedhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali za kimofosintaksia. Baadhi ya dosari hizi ni kama zifuatazo:

4.1 Vipatanishi vya Kisarufi vya Nomino Visivyo Sahihi

Data zilizokusanya kwa kutumia uandishi wa insha, usaili na ushuhudiaji zinaonesha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari za vipatanishi vya nomino tofauti visivyo sahihi. Ilibainika kuwa wajifunzaji walitumia vipatanishi

vya kisarufi visivyo kuwa sahihi kurejelea nomino mbalimbali za ngeli tofauti. Baadhi ya dosari hizo zinabainika katika Insha Na. 4.1 na Dondoo Na. 4.1 kutoka katika moja ya simulizi za watoataarifa.

Insha Na. 4. I

.....Siku...Ambaye...sitasaha...Daima.....
.....Jina.langu..ni..Nsamba..Usama..kutoka.shule.ya..kijeshi.....
.....Mbarara.....
.....Nilikuwa...siku.maja...nilikuwa...katika...dalasani.tya.inc.
.....kidata.cha...(*4.c)...Ni.lisaa...tangezo...enoia...wanafunzi.....
.....walitaka.ku.ingia.chikundi...kyo..kiswahili..katika..shule.yote.
.....Nilika..chini..dakika...et.coma.mbilli.lil/chochoba..nhaesma..wacha
.....niliesma..wacha..niende..kuona..mipango..jinaendelea..Katika...
.....chikundi..kicho..Nilinda..na..rafiki..yangu..anaitwa..Ayeshale.
.....Sephata..Sadat..Kufika..huka..nito.niliona..swatu.wingiwall..Ingia
.....Namim..nilivaliza..rafiki..yangi..("tingi.ye..ndoni..?")..nilikia...
.....wanafunzi..wanapiga..kelcie..wanaitija.langu.."Usama..usama!"
.....niliwaulizo..shida.gani..wallsema..tunafurahi.....

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari -Machi, 2023)

Data hapo juu inadhihirisha kuwa mjifunzaji alifanya dosari za kimofosintaksia za kutumia vipatanishi vya kisarufi visivyo sahihi. Dosari zinazobainika katika data hii zitajadiliwa baada ya kuwasilisha data kutokana na masimulizi ya wajifunzaji ili kuepuka urudiaji wa hoja.

Kutokana na data zilizokusanya kwa kutumia ushuhudiaji, matini simulizi za wajifunzaji zilikuwa na dosari za kimofosintaksia za matumizi yasiyo sahihi ya vipatanishi vya kisarufi. Kwa mfano, kwa kutumia alama (*), tumebainisha dosari zinazojitekeza katika masimulizi hayo ya mjifunzaji kama inavyoonekana katika Dondoo Na. 4.1.

Dondoo Na. 4.1

Siku mvua *elinyesha sana na gari nyingi *zilikuwa *zinaterera sana kwa muda. Tulienda polepole lakini mbele tulipata ajali mbaya. Gari *imegonga ngombe kwa sababu ngombe *ilikuwa katikati barabarani. Sehemu iyo *elikuwa na ngombe *nyingi *zikitoka huku na huku...

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Kutokana na data hizi (Insha Na. 4.1 na Dondoo Na. 4.1), dosari za kimofosintaksia zilizofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari kuhusiana na matumizi ya vipatanishi vya kisarufi visivyo sahihi zinaoneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Vipatanishi vya Kisarufi Visivyo Sahihi

Na.	Dosari	Kwa Kiswahili Sanifu
a)	Tangazo *enaita	Tangazo linaita
b)	Mipango *jinaendelea	Mipango inaendelea
c)	Wantu *wingi	Watatu wengi
d)	Wantu *wengine	Watatu wengine
e)	Chakula *elikuwa	Chakula kilikuwa
f)	Gari *elienda	Gari lilienda
g)	Viyato *nzuri	Viyato vizuri
h)	Gari *zilikuwa	Magari yalikuwa
i)	Ng'ombe *ilikuwa	Ng'ombe alikuwa
j)	Ng'ombe nyingi *zikitoka huku	Ng'ombe wengi wakitoka

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Tukichunguza data katika Jedwali Na.1, tunaona kuwa wajifunzaji walifanya dosari kwa kutumia vipatanishi visivyokuwa sahihi kwa nomino tofauti kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Katika Mfano (a), kunabainika dosari ya matumizi ya kipatanishi kisicho sahihi {e-} badala ya {li-} kwa nomino ya ngeli ya LI-YA (kwa kuzingatia uainishajji wa kisintaksia) katika hali ya umoja. Katika tingo hii, mjifunzaji anashindwa kutumia kipatanishi sahihi cha nomino *tangazo* ambayo ni ya ngeli ya LI-YA. Hivyo, kipatanishi sahihi ambacho kilipaswa kutumiwa ni {li-}.

Katika Mfano (b), kuna dosari ya matumizi ya kipatanishi {ji-} badala ya {i-} kwa nomino ya ngeli ya U-I katika wingi. Katika tingo hii, mjifunzaji alishindwa kutumia kipatanishi sahihi cha nomino *mipango*. Hivyo, matokeo ya kushindwa kutumia kipatanishi sahihi ni kutunga tingo isiyo sahihi *mipango jinaendelea* badala ya *mipango inaendelea*.

Aidha, dosari za matumizi ya vipatanishi visivyo sahihi pia zinabainika katika mifano (c) na (d), ambapo kuna matumizi ya kipatanishi {wi-} badala ya {wa} kwa nomino za ngeli ya A-WA.

Katika tingo kirai nomino *wantu wingi* na *wantu wingine*, mbali na nomino kutokuandikwa kwa usahihi, yaani, *wantu*, badala ya *watu*, kipatanishi {wi} kilichotumiwa si sahihi. Nomino hii ni ya ngeli ya A-WA, na kwa hivyo, vipatanishi vyake sahihi ni {a-} na {wa-} katika umoja na wingi mtawalia. Kwa hiyo, wajifunzaji walipaswa kutumia kipatanishi {wa} kufanya upatanisho sahihi wa nomino *watu* na kivumishi kiidadi *-ingi* na *ingine*. Hivyo, kwa usahihi mjifunzaji alipaswa kusema *watu wengi* badala ya *wantu wingi* na *watu wengini*. Kimuundo, kipatanishi cha nomino za ngeli ya A-WA katika wingi ni {wa-} na kikiunganishwa na mzizi wa kiidadi *-ingi/-ingine*, irabu [a] huunganishwa na [i] na kuwa [e]. Yaani (wa + ingi= wengi, wa + ingine= wengine).

Mfano (e) unaonesha dosari kutokana na matumizi ya kipatanishi {e-} kisicho sahihi katika upatanishi wa nomino *chakula* ambayo ni ya ngeli ya KI-VI. Vipatanishi vya nomino za ngeli ya KI-VI ni {ki-} na {vi-} katika umoja na wingi. Kwa mujibu wa Mfano (e) katika Jedwali Na. 1, inadhihirika kuwa wajifunzaji pia walifanya dosari kwa kushindwa kutumia vipatanishi sahihi vya ngeli ya KI-VI, mathalani, katika tingo *chakula elikuwa nzuri* badala ya *chakula kilikuwa kizuri*.

Hali kadhalika, katika mifano (f) na (h), nomino *gari* ya ngeli ya LI-YA, inarejelewa kwa kutumia kipatanishi kisicho sahihi {e-} na {zi-} katika umoja na wingi badala ya {li-} na {ya-}. Nomino gari ni ya ngeli ya LI-YA, ambapo katika ngeli hii, vipatanishi sahihi ni {li-} katika umoja na {ya-} kwa wingi. Hivyo, wajifunzaji kutumia vipatanishi {e-} na {zi-} na

kurejelea nomino za ngeli ya LI-YA si sahihi. Sambamba na hayo, katika mifano (i) na (j) kuna dosari za matumizi ya vipatanishi “i/zi” badala ya “a/wa” kwa nomino za ngeli ya {A-WA}.

Data za utafiti huu pia zinaonesha kuwa wajifunzaji walifanya dosari kwa kutumia vipatanishi {i} na {zi} kurejelea nomino za ngeli ya {A-WA}, ambayo hujumuisha nonimo zote zinazotaja viumbi hai, wakiwamo wanyama. Kwa mfano, katika data iliyonukuliwa kutokana na masimulizi ya mjifunzaji, kama inavyobainishwa katika Jedwali Na. 1, katika Mfano (i), mjifunzaji alisema “*ngombe ilikuwa*” badala ya “*ng’ombe alikuwa*”. Vilevile, katika Mfano (j) mjifunzaji alisema, “*ngombe nyangi zikitoka huku*” badala ya “*ng’ombe wengi wakitoka huku*”. Kwa hiyo, kutokana na mifano hii, inabainika kuwa wajifunzaji waliirejelea nomino ng’ombe katika sentensi kwa kutumia kipatanishi “i” badala ya “a” katika umoja na “zi” badala ya “wa” katika wingi na kuisababishia tingo nzima kutokuwa sahihi kimofosintaksia.


Kwa ujumla, katika kipengele hiki, imebainika kuwa watoataarifa wajifunzaji walifanya dosari mbalimbali za matumizi yasiyo sahihi ya vipatanishi vya kisarufi. Aidha, imebainika kuwa wajifunzaji wanakosa ujuzi wa kutumia viambishi vya upatanishi wa kisarufi vya nomino za ngeli tofauti. Hali hii inawafanya washindwe kuvitumia vipatanishi hivyo kwa usahihi. Matokeo ya utafiti huu yanashabihiana na matokeo ya utafiti wa Vincent (2019) katika utafiti wake uliochunguza dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii ya Wairaki. Katika utafiti huo, Vincent pia alibainisha kuwa dosari za upatanishi wa kisarufi zilibainika sana katika tingo za wajifunzaji kuliko dosari nyinginezo. Hali hii ilidhahirisha kuwa wajifunzaji walikosa ujuzi kuhusu matumizi ya kipengele hiki cha sarufi.

Matokeo haya ya utafiti yanaafikiana na mhimili mkuu wa Nadharia ya Usasanyuzi Dosari amba ni utendaji. Kwa mujibu wa mhimili huu, Corder (1967) anaeleza kuwa katika ujifunzaji lugha, dosari zinazofanywa na wajifunzaji hutokana na wao wenyewe kukosea kanuni za lugha wanazojifunza kutokana na ukosefu wa ujuzi kuhusu kanuni hizo. Kwa kuchunguza dosari zilizobainishwa katika Jedwali Na. 1, ni dhahiri kwamba wajifunzaji hawakujua ni vipatanishi vipi sahihi ambavyo vilipaswa kutumiwa kurejelea nomino za ngeli tofauti walizozitumia katika tingo zao.

4.2 Matumizi ya Viambishi Ngeli za Nomino Visivyo Sahihi

Kutokana na data za uwandani zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha na ushuhudiaji, ilibainika kuwa wajifunzaji pia walifanya dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya viambishi vya nomino vya idadi ya umoja na wingi. Kwa mfano, katika Insha Na. 4.2 na Dondoo Na. 4.2 kutoka katika simulizi mojawapo, dosari za aina hii zinajidhahirisha.

Insha Na. 4.2



Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Data hii inabainisha dosari za kimofosintaksia za matumizi ya viambishi vya nomino vya idadi ya umoja na wingi visivyo sahihi zilizofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili.

Hali kadhalika, kutokana na data zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, data zilizorekodiwa kutokana na masimulizi ya wajifunzaji pia zilizidhihirisha kuwepo kwa dosari za kutumia viambishi vya nomino visivyo sahihi. Kwa mfano, kulikuwa na masimulizi ya mjifunzaji akiigiza kuhusu kampeni za kugombea cheo katika jamii. Alisema:

Dondoo Na. 4.2

Ee Paulo oye, oye, oye, pigia Paulo voti yako. Mimi iko hapa kama *kifunguo cha maisha yanyu. Mkimpa voti *mabarara yatakuwa mazuri, *mashule

mazuri yatajenga, *gari za kwenda na wagonjwa naleta na *mavitu mazuri sana na *mingi itakuja. Ee Paulo oye...

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Kwa ujumla, data hizi zinadhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari za kimofosintaksia za matumizi ya viambishi vya nomino visivyo sahihi. Matumizi ya viambishi hivyo yaliathiri matumizi ya maneno mengine katika tungo na kusababisha dosari za kimofosintaksia. Mifano ya dosari za matumizi ya viambishi vya nomino visivyo sahihi inaoneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na. 2: Viambishi vya Nomino Visivyo Sahihi

Na.	Dosari	Kwa Kiswahili Sanifu
a)	<u>*Kifunguo kyake</u>	<u>Ufunguo wake</u>
b)	<u>*Nkufuli ifunga mlango</u>	<u>-Kufuli limefungwa mlangoni</u>
c)	<u>*Bagenyi bote</u>	<u>Wageni wote</u>
d)	<u>*Chikundi ya wanawake</u>	<u>- Kundi la wanawake</u>
e)	<u>*Kifunguo cha maisha</u>	<u>Ufunguo wa maisha</u>
f)	<u>*Mabarabara mazuri yatakuwa</u>	<u>-Barabara nzuri zitakuwa</u>
g)	<u>*Mashule mazuri yatakuwa</u>	<u>-Shule nzuri zitakuwa</u>
h)	<u>*Mavitu mazuri</u>	<u>Vitu vizuri</u>
i)	<u>*Gari za kwenda</u>	<u>Magari ya kwenda</u>

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Data zilizomo katika Jedwali Na. 2 zinabainisha dosari za matumizi ya viambishi vya nomino visivyo sahihi. Wajifunzaji walipotumia viambishi vya nomino visivyo sahihi katika tungo zao, viambajengo vingine katika tungo hizo pia viliathiriwa na kusababisha dosari

za kimofosintaksia. Dosari hizo zinafafanuliwa zaidi katika aya zifutazo.

Katika mifano (a) na (e), kuna dosari kutokana na matumizi ya kiambishi {ki-} badala ya {u-}. Katika mifano hii, wajifunzaji walifanya dosari za kutumia

kiambishi {ki} badala ya {u-} kwa neno *-funguo* na kusema *kifunguo kyake* na *kifunguo cha maisha* badala ya *ufunguo wake* na *ufunguo wa maisha*. Kutumia kiambishi hicho kuliathiri matumizi ya kivumishi kimilikishi katika tungo. Mtoataarifa badala ya kutumia kihusishi {wa-} yaani, *ufunguo wake* na *ufunguo wa maisha*, alitumia *cha* na tungo nzima kuwa *kifunguo chake* na *kifunguo cha maisha*, ambazo si tungo zilizo sahihi kimofosintaksia.

Katika Mfano (b), mjifunzaji alipachika kiambishi {n-} katika mzizi wa neno *kufuli*. Nomino *kufuli* katika Kiswahili haina viambishi vya umoja. Kwa hiyo, kuambisha nomino hii na kiambishi {n-} ni dosari.

Aidha, katika Mfano (c), kuna dosari ya matumizi ya kiambishi awali kisicho sahihi {ba-} badala ya {wa-}. Katika tungo hii, wajifunzaji walifanya dosari kwa kutumia kiambishi kisichokuwa sahihi cha ngeli ya M/MU-WA (kwa kuzingatia kigezo cha kimofolojia) na kusema *bagenyi bote* badala ya *wageni wote*. Katika kirai nomino hiki, matumizi ya kiambishi kisicho sahihi yaliathiri matumizi ya kivumishi kiidadi kilichotumiwa. Badala ya kutumia *wote*, mjifunzaji huyo alisema *bote* na kufanya tungo kuwa *bagenyi bote* badala ya *wageni wote*. Kwa kufanya hivyo, mjifunzaji huyo alifanya dosari ya kimofosintaksia.

Tukichunguza Mfano (d), tunaona kwamba kuna dosari ya matumizi ya kiambishi awali kisicho sahihi {chi-} kwa nomino kundi ambayo katika umoja haibebi kiambishi awali. Matumizi ya kiambishi hicho yaliathiri kihusishi kilichotumiwa katika upatanisho wa nomino hiyo na maneno mengine. Yaani, *chikundi ya wanawake* badala ya *kundi la wanawake*.

Pamoja na hayo, katika mifano (f) na (g), kuna dosari za matumizi ya kiambishi {ma} kwenye nomino zisizo na kiambishi awali chochote cha idadi. Katika mifano (f) na (g), kiambishi awali {ma-} kilipopachikwa kwenye nomino *barabara na shule*, kiliathiri matumizi ya viambajengo vingine kama vile kivumishi. Kwa mifano, badala ya kivumishi kuwa *nzuri*, wajifunzaji walisema *mazuri*. Aidha, kipatanishi kilichotumiwa kupatanisha nomino hizo na kitenzi pia kiliathiriwa na kuwa {ya-} badala ya {zi-}, ambacho si sahihi. Pia, katika Mfano (h), kiambishi awali {ma-} kilipachikwa kimakosa katika nomino *vitu* na hili liliathiri kipatanishi cha kisarufi kilichotumiwa, yaani; badala ya kusema *vitu*

vizuri, mjifunzaji alisema *mavitu mazuri* ambayo si sahihi.

Isitoshe, katika Mfano (i), kunadhihirika dosari ya kudondosha kiambishi awali cha nomino *gari* ambayo katika muktadha wa sentensi inamotumiwa, inaonekana kuwa mjifunzaji alilenga kuitumia kwenye wingi. Hivyo, tungo *gari za kwenda* si sahihi. Badala yake, mjifunzaji alitakiwa kutumia kiambishi awali {ma-} na kihisishi {ya} ili kutunga tungo sahihi, *magari ya kwenda*.

Matokeo ya utafiti katika kipengele hiki yanaonesha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda pia walifanya dosari za kimofosintaksia kutokana na matumizi ya viambishi vya nomino visivyo sahihi. Imebainika kwamba matumizi ya viambishi vya nomino visivyo sahihi yanasaababisha kuathiriwa kwa upatanisho wa nonimo hizo na maneno mengine katika virai na sentensi, hivyo kutokea kwa dosari za kimofosintaksia.

Matokeo haya ya utafiti yanaafikiana na mawazo ya Guerois, Rozzen, na Lutz (2017) ambao wanabainisha kuwa kipengele cha uambishaji ni cha kimofosintaksia. Kwa maana hii, viambishi vya nomino vinaathiri tungo kimofosintaksia. Kama inavyooneshwa katika sehemu hii, wajifunzaji kukosa uujuzi kuhusu viambishi sahihi vya nomino za ngeli tofauti kuliwasababishia kushindwa kuhusisha nomino hizo na maneno mengine waliyoyatumia katika tungo kwa usahihi. Hali hii inadhihirisha ukweli wa mawazo ya Corder (1967) katika Nadharia ya Usasanyuzi Dosari kuwa, dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa L2 husababishwa na wajifunzaji wenyewe kukosea kanuni za matumizi ya lugha hiyo. Tukichunguza tungo ambazo zimebainishwa katika Jedwali Na. 2, ni dhahiri kuwa wajifunzaji hawajua ni viambishi gani vya nomino walivyopaswa kuvitumia katika tungo zao.

4.3 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vielezi

Data za utafiti huu pia zinadhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari za kimofosintaksia kwa kutumia vielezi visivyo sahihi katika sentensi wanazozitunga. Kutokana na data zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha, usaili na ushuhudiaji, ilibainika kuwa wajifunzaji walifanya dosari kwa kushindwa kutumia vielezi sahihi. Mifano ya dosari hizo inabainika katika Insha Na. 4.3 na Dondoo Na. 4.3.

Insha Na. 4.3

The handwritten text is a composition in Swahili. It discusses various concepts such as 'Siku Ambayo Sitasahau', 'Shulen', 'Ofisini', 'Mwalimu', 'Barabarani', 'Amaenda', 'Shokoni', 'Nyumbani', 'Garini', 'Kudarasa', 'Kuingiamu', 'Niliogopa', 'Nyumbani', 'Shule', and 'Nyumbani'. The text is written in a cursive style with some corrections and additions.

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Dondoo Na. 4.3

Nilianzia *katika shulen kidatoni moja kujifunza lugha ya swahili. Nilifika *katika shulen niliona wanafunzi wingi *katika shulen. Nilifika *kudarasa na wanafunzi alikuwa wingi sana. Niligopa *kuingiamu nkataka kwenda *katika nyumbani. Hapo naona kanisa *mushule nikataka kwenda *kukanisa nijifiche...

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari-Machi, 2023)

Katika data hizi, kunabainika dosari za kimofosintaksia za matumizi ya vielezi visivyo sahihi. Mifano ya dosari za aina hii inabainishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 3.

Jedwali Na. 3: Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vielezi

Na.	Dosari	Kwa Kiswahili Sanifu
a)	Nilianzia* <u>katika nyumbani</u>	Nilianzia nyumbani
b)	Nilifika * <u>Katika shulen</u>	Nilipofika <u>shulen</u>
c)	* <u>Katika ofisini ya muoalimu mkwu</u>	Ofisini mwa mwalimu mkuu
d)	* <u>Tulikoa katika barabarani</u>	Tulipokuwa barabarani
e)	* <u>Amaenda katika shokoni</u>	Ameenda sokoni
f)	* <u>Katika garini</u>	Garini /kwenye gari
g)	Nilifika * <u>kudarasa</u>	Nilipofika <u>darasani</u>
h)	Niligopa * <u>kuingiamu</u>	Niliogopa <u>kuingia ndani</u>
i)	Niliona kanisa <u>mushule</u>	Niliona kanisa <u>shulen</u>

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Mifano inayobainishwa katika Jedwali Na.3 ni dosari za kimofosintaksia za matumizi yasiyo sahihi ya vielezi. Dosari hizi zimefanuliwa zaidi katika aya zinazofuata.

Tukichunguza mifano (a), (b), (c), (d), (e) na (f), tunaona kwamba wajifunzaji walitumia *katika* na {-ni} kuelezea mahali yaani, nyumbani, shulen, ofisini, barabarani, sokoni na garini. Katika sarufi ya Kiswahili, kwa au katika inapoambatana na nomino kuelezea mahali husika, mofu kiambishi tamati {-ni} hakitumiwi. Kiambishi hicho hutumiwa peke yake na wala si kwa pamoa na *kwa* au *katika*.

Mbali na hayo, Mfano (g) unaonesha kwamba, wajifunzaji walifanya dosari walipotumia mofu {ku}


kwa maana ya *ndani*, yaani, *darasani*. Wajifunzaji badala ya kutumia mofu hiyo ambayo si sahihi, walipaswa kutumia kiambishi tamati {-ni} kwa mzizi wa nomino darasa (darasa + ni =darasani) na wala si vinginevyo kama walivyofanya. Katika Mfano (h), mjifunzaji alitumia mofu {-mu} kama kiambishi tamati na kukipachika katika kitende *kuingia* na kusema *niliogopa kuingiamu* badala ya *niliogopa kuingia ndani*. Aidha, katika Mfano (i), mjifunzaji alisema *niliona kanisa mushule* badala ya *niliona kanisa shulen/ ndani ya shule*. Katika tungo hii, mofu {-mu} ambayo ilipachikwa kwenye mzizi wa nomino katika sehemu ya kiambishi awali si sahihi. Badala yake, mjifunzaji angetumia kiambishi tamati {-ni} na kutunga tungo sahihi, yaani, *niliona kanisa shulen*.

Kwa mujibu wa matokeo haya ya utafiti, ni dhahiri kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya vielezi vinavyotokana na nomino. Tungo zilizotungwa na wajifunzaji kuhusiana na kipengele hiki zimedhihirisha kuwa wajifunzaji walikosa ujuzi wa kutumia vielezi vya mahali vya aina hii.

4.4 Matumizi ya Virejeshi Visivyo Sahihi

Data zilizokusanywa kutoka uwandani pia zinadhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari za matumizi ya virejeshi visivyo sahihi. Mifano ya tungo zenye dosari za aina hii inajidhihirisha katika Insha Na. 4.4 na Dondoo Na. 4.4.

Insha Na. 4.4



Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Aidha, data kutokana na uandishi wa insha pia zinaonesha kuwapo kwa dosari za matumizi yasiyo sahihi ya virejeshi katika tungo za wajifunzaji. Kwa mfano, katika masimulizi ya mjifunzaji mmoja wa kidato cha tano kuhusu riwaya ya *Kufa Kuzikana* katika somo la fasihi, alitoa majibu akitumia virejeshi vya nomino mbalimbali visivyo kuwa sahihi. Alisema:

Dondoo Na. 4.4

Riwaya ya *Kufa Kuzikana* ni riwaya ili*yeandikwa na Ken Walibora. Ni riwaya *ambaye inazungumzia Akida na Tim wali*yokuwa na urafikiuli*yokuwa wa dhati sana. Hata kama Akida

alipata matatizo amba*zo aliletewa na Tim lakini Urafiki yao ulisonga mbele. Kwa mfano, Tamari aliwa na tabia mbaya na siki moja alidanganya kwamba Akida alitataka kumbaka. Lakini hayo aliomfanyia Akia yaliku bure. Maana urafiki yao ulizidi kuendelea...

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Data hii inabainisha dosari za kimofosintaksia zinazotokana na matumizi ya virejeshi visivyo sahihi. Mifano zaidi ya tungo zenye dosari za aina hii inaoneshwa katika Jedwali Na. 4.

Jedwali Na. 4: Matumizi Yasiyo Sahihi ya Virejeshi

Na.	Dosari	Kwa Kiswahili Sanifu
a)	Wanafunzi amba*yo	Wanafunzi ambao
b)	Mwanafunzi amba*yo	Mwanafunzi ambaye
c)	Gari amba*yo	Gari ambalo
d)	Kijiji amba*yo	Kijiji ambacho
e)	Akuna kitu kili*yotokeya	Hakuna kitu kilichotokea
f)	Riwaya ili*yeandikwa	Riwaya ilioandikwa
g)	Riwaya amba*ye	Riwaya ambayo
h)	Akida na Tim wali*yokuwa	Akida na Tim waliokuwa
i)	Urafiki uli*yokuwa	Urafiki ambao
j)	Matatizo amba*zo	Matatizo ambayo

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Data za Jedwali Na. 4 zinaonesha kuwa wajifunzaji walifanya dosari kwa kutumia virejeshi

visivyo kuwa sahihi kurejelea nomino za ngeli tofauti. Dosari hizo zimeelezwa katika aya zinazofuata.

Katika Mfano (a), mjifunzaji alitumia kirejeshi kisicho sahihi {-yo} kurejelea nomino *wanafunzi* ya ngeli ya A-WA. Aidha, katika (b), mjifunzaji alitumia kirejeshi hichohicho kurejelea nomino hiyo kwa umoja. Kiambishi hiki si sahihi kutumiwa kurejelea nomino za ngeli hii. Nomino za ngeli hii hutumiwa kirejeshi {-ye} katika umoja na {-o} katika wingi. Kwa hivyo, katika Mfano (a), mjifunzaji alipaswa kutumia kirejeshi {-o} na kusema, *wanafunzi ambao*. Vilevile, katika Mfano (b), alipaswa kutumia kirejeshi {-ye} na kusema, *mwanafunzi ambaye*.

Katika Mfano (c), kirejeshi (yo), kinatumiwa kurejelea nomino ya Ngeli ya LI-YA katika umoja, yaani, *gari*. Katika ngeli hii, kirejeshi cha umoja ni {-lo} na cha wingi ni {yo}. Hivyo, mjifunzaji alipaswa kutumia kirejeshi {-lo} na kusema *gari ambalo*.

Hali kadhalika, katika Mfano (d), kuna dosari ya kutumia kirejeshi kisicho sahihi {-yo} kurejelea nomino *kijiji ambayo* ni ya ngeli ya KI-VI. Katika ngeli hii, nomino hurejelewa kwa kutumia kirejeshi {-cho} katika umoja na {-vyo} katika wingi. Kwa hiyo, mjifunzaji alipaswa kutumia kirejeshi {-cho} katika tungo hii na kusema, *kijiji ambacho*. Pia, katika Mfano (e), tungo *akuna kitu kiliyotokea* si sahihi kutokana na matumizi ya kirejeshi kisicho sahihi {-yo}. Kirejeshi sahihi ambacho kilipaswa kutumiwa ni {-cho} na tungo sahihi ambayo ilipaswa kutungwa ni *hakuna kitu kilichotokea*.

Katika mifano (f) na (g), kirejeshi {-ye} kimetumiwa kurejelea nomino *riwaya* badala ya {yo}. Katika sarufi ya Kiswahili, kirejeshi {-ye-} hutumiwa kurejelea viumbe vyenye uhai katika hali ya umoja. Kwa hiyo, kukutumia kurejelea nomino *riwaya* si sahihi. Badala yake, mjifunzaji angetumia kirejeshi {-yo-} na kutunga tungo sahihi, yaani, *riwaya ambayo*.

Isitoshe, katika Mfano (h), kirejeshi {-yo-} kimetumiwa kurejelea *Akida na Tim* ambayo ni watu/

viumbe hai. Hii ina maana kuwa, kwa kuwarejelea wahusika hawa, mjifunzaji alipaswa kutumia kirejeshi {-o-} cha Ngeli ya A-WA. Hali kadhalika, katika Mfano (d), nomino *urafiki* inarejelewa kwa kutumia kirejeshi {-yo}, yaani, *urafiki uliyokuwa* badala ya mjifunzaji kutumia kirejeshi {-o-} na kusema, *urafiki uliokuwa*.


Vilevile, katika Mfano (e), kirejeshi {-zo-} kilitumiwa kurejelea nomino *matatizo* kwa kusema *matatizo ambazo* badala ya kutumia {-yo-} na kusema *matatizo ambayo*. Kwa hiyo, kutokana na mifano hii, ni dhahiri kuwa wajifunzaji hufanya dosari za kimofosintaksia kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya virejeshi vya nomino husika katika tungo.

Kwa mujibu wa matokeo haya ya utafiti, inabainika kwamba wajifunzaji katika eneo tajwa hawajui kanuni za matumizi ya virejeshi vya nomino za ngeli tofauti katika lugha ya Kiswahili. Hii inawasababishia kufanya dosari kutokana na kukosa kanuni hizo za matumizi ya kipengele hiki cha kisarufi. Hali hii inashabihiana na msingi mkuu wa Nadharia ya Usasanyuzi Dosari usemao kwamba, dosari zinazofanywa na wajifunzaji lugha hutokana na wajifunzaji kukosea kanuni za lugha wanayojifunza.

5.2.5 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Njeo

Data zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha na ushuhudiaji zinadhahirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari za matumizi yasiyo sahihi ya njeo. Ilibainika kuwa wajifunzaji walichanganya njeo kimatumizi. Sentensi walizozitunga zilitumia njeo {-ta-}, {-me-} na {-na-} badala ya {-li-} ya wakati uliopita, {-lime-} badala ya {-li-} na nyinginezo kama inavyoonekana katika Insha Na. 4.5 na madondoo kutoka kwa masimilizi ya wajifunzaji.

Insha Na. 4.5



Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Katika data hii, kunabainika dosari za matumizi yasiyo sahihi ya njeo. Aidha, kutokana na data za ushuhudiaji, dosari za matumizi yasiyo sahihi ya njeo zinajibainisha. Kwa mfano, katika masimulizi wakati wa usaili, mjifunzaji mmoja katika kusimulia hadithi kuhusu siku ambayo hataisahau daima, alisema: “*Siku ambayo *sinasahau ni siku mimi na mjomba *tunaenda mjini. *Tunaona wantu wingi, gari nydingi na mayumba ndefu sana. *Ninauliza mjomba kwa nini gari ni nydingi na mjomba *anasema mjini ni ya watu tajiri.*” Hali kadhalika, katika simulizi ya mjifunzaji wa kidato cha tano kuhusu umuhimu wa baba nyumbani, alisema; *umuhimu wa baba nyumbani ni *alikuleta chakula nyumbani, *alilipa pesa ya school fees*, alikukeep watoto na mama nyumbani na **alimeleta security*.

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Kadhalika, katika usaili mjifunzaji wa kidato cha sita alitumia njeo isiyokuwa sahihi. Dosari

zilizofanywa na mjifunzaji huyo zimeoneshwa katika Dondoo Na. 4.5.

Dondoo Na. 4.5

Akida **alimekuwa rafiki* wake wa zamani na dhati na Tim. Hiki kinaonekana alikuwa Mkanju na Tim Mkorosho na Wakorosho **watasumbua* Wakanju, hata baba wa Tim **alimeua* baba wa Akida lakini Akida **alimesamehe* Tim rafiki. Pia Tim anapeleka na Akida kwa siku ya kuzawadiwa lakini Tim anakuwa na akili kidogo masomoni...

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Data katika madondoo tajwa hapo juu zinadhihirisha dosari mbalimbali za matumizi yasiyo sahihi ya njeo ambazo zimebainishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5: Matumizi ya Njeo Zisizo Sahihi

Na.	Dosari	Kwa Kiswahili Sanifu
a)	<i>*siku hiyo na tembea</i>	Siku hiyo nilitembea
b)	<i>Mimi nimetembea</i>	Mimi nilitembea
c)	<i>Nyanya alime uliza</i>	Nyanya aliniuliza
d)	<i>Tunaenda mjini</i>	Tulienda mjini
e)	<i>Tunaona wantu wingi</i>	Tuliona watu wengi
f)	<i>Ni meambia wazazi wangu</i>	Niliwaambia wazazi wangu
g)	<i>Akida alimekuwa rafiki</i>	Akida alikuwa rafiki
h)	<i>Ni *taenda shulen</i>	Nilijenda shulen
i)	<i>A *limesamehe</i>	Alimsamehe
j)	<i>A *likununua chakula</i>	Hununua chakula
k)	<i>A *lilipa pesa ya school fees</i>	Hulipa karo
l)	<i>A *likuleta security nyumbani</i>	Huleta usalama nyumbani

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari-Machi, 2023)

Kutokana na data katika Jedwali Na. 5, inabainika kuwa wajifunzaji walifanya dosari za matumizi ya njeo zisizo sahihi. Dosari hizi zinafafanuliwa zaidi katika aya zinazofuata.

Katika mifano (a), (d) na (e) wajifunzaji walitumia njeo ya wakati uliopo {-na-} badala ya kutumia njeo {-li-} ya wakati uliopita na kuzifanya sentensi zilizotarajiwa kuwa katika wakati uliopita, kuwa za wakati uliopo. Kwa mfano, katika Mfano (a), mjifunzaji anasema, *siku hiyo na tembea* badala ya *siku hiyo nilitembea*. Katika Mfano (d), mjifunzaji anasema, *tunaenda mjini* badala ya *tulienda mjini* na katika Mfano (e), mjifunzaji anasema *tunaona watu wingi* badala ya *tuliona watu wengi*. Tungo hizi zinadhihirisha matumizi ya njeo isiyu sahihi ambapo watoataarifa walitumia njeo ya wakati uliopo kusimulia hadithi badala ya njeo ya wakati uliopita. Kwa kufanya hivyo, hali hii ilipotosha ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa.

Mbali na hayo, katika mifano (b) na (f), watoataarifa wajifunzaji walitumia njeo ya hali timilifu


{-me-} badala kutumia njeo ya wakati uliopita {-li-}. Walitunga tungo *mimi nimetembea* na *nimeambia wazazi wangu* ambazo zinatoa taarifa katika hali timilifu badala ya kutumia njeo {-li-} na kutunga sentensi sahihi zilizo katika njeo iliyopita, yaani, *mimi nilitembea* na *niliwaambia wazazi wangu*.

Vilevile, katika mifano (c), (g), na (i), kuna dosari za matumizi ya {-lime-} badala ya {-li-} ya wakati uliopita. Katika Mfano (c), mjifunzaji alisema, *nyanya alime uliza* badala ya *nyanya aliniuliza*. Katika Mfano (g), mjifunzaji alisema, *Akida alimekuwa rafiki* badala ya *alikuwa rafiki*. Katika Mfano (i), tungo *alimesamehe* si sahihi. badala yake mjifunzaji angesema, *alimsamehe*.

Mifano (j), (k) na (l) inadhihirisha dosari za matumizi yasiyo sahihi ya njeo ya mazoea. Katika tungo hizi, yaani, *alikununua chakula*, *alikulipa pesa ya school fees* na *alikuleta security nyumbani*, wajifunzaji walipaswa kutumia njeo ya mazoea {-hu} katika kutaja majukumu ya baba nyumbani ambayo hutekelezwa kila siku.

Kwa mujibu wa matokeo haya ya utafiti, imebainika kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari za matumizi yasiyo sahihi ya njeo. Hii ni kutokana na tungo mbalimbali za wajifunzaji ambazo baada ya kuchanganuliwa katika sehemu hii zimeddihirisha kuwa wajifunzaji walikosea kanuni za matumizi ya njeo kwa kushindwa kutambua mofu sahihi iliyopaswa kutumiwa kulingana na muktadha wa wakati husika wa ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa.

Ama kwa hakika, matokeo haya ya utafiti pia yanashadidiwa na matokeo ya utafiti wa Vincent (2019, 2020) uliohusu kuchunguza dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii ya Wairaki. Katika utafiti huo, Vincent alibaini pia kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika jamii hiyo walishindwa kutumia njeo sahihi katika tungo za Kiswahili walizozitunga. Japokuwa tafiti hizi zilifanyika katika jamii tofauti, matokeo yake yanaafikiana na mawazo ya Corder (1967) katika Nadharia ya Usasanyuzi Dosari kuwa, dosari zinazofanywa na wajifunzaji lugha hutokana na wajifunzaji kukosea kanuni za lugha lengwa.



Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Dondoo Na. 4.6.1

...wakati *hiyo, mama wangu alikuwa amegonjwa sana. Sisi jirani yote ni watu mbaya sana wana fitina katika kijiji hii. Alakini mama anagonjwa sana. Nilikuona nkasema wacha niende kwa nyumbani *hilo. Ninakuwa watu kusaidi mimi mama yangu. *Hilo siku inakuwa baba anaenda mjini Mbarara anachelewa huko. Muda hiyo ya Lockdown polisi anakamata watu sababu ya Korona...

Jedwali Na .6.1: Vionyeshi Visivyo Sahihi

Na.	Dosari	Kwa Kiswahili Sanifu
a)	Insha huu	Insha hii
b)	Siku huu	Siku hiyo
c)	Maswali huu	Maswali hayo

4.6 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vivumishi

Kutokana na data za utafiti zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha, usaili pamoja na ushuhudiaji, ilibainika kuwa, mionganoni mwa dosari zilizofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda, kulikuwamo dosari za matumizi yasiyo sahihi ya vivumishi. Dosari hizo zinaleezwa katika vipengele vidogo vinavyofuata.

4.6.1 Matumizi ya Vionyeshi Visivyo Sahihi

Kwa mujibu wa data za utafiti huu, ilibainika kuwa wajifunzaji pia hufanya dosari kutokana na matumizi ya vionyeshi visivyo sahihi kulingana na nomino inayorejelewa. Hii inabainika katika sampuli za kazi za wajifunzaji zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha katika data za usaili na ushuhudiaji ambazo zilidhihirisha kutatizika kwa wajifunzaji kuhusu matumizi ya vionyeshi. Mifano ya dosari za aina hii imebainishwa katika Insha Na. 4.6.1 na Dondoo Na.4.6.1 kutoka katika masimulizi ya wajifunzaji.

Insha Na. 4.6.1

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Data za Insha Na. 4.6.1 na Dondoo Na. 4.6.1 zinaonesha kwamba wajifunzaji walifanya dosari kwa kutumia vionyeshi visivyo kuwa sahihi. Data za vionyeshi visivyo sahihi zimeoneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 6.1.

d)	Karatasi huo	Karatasi hiyo
e)	<i>Wakati *hiyo</i>	Wakati huo
f)	<i>Daktari *huo</i>	Daktari huyo
g)	<i>Muda *hii</i>	Muda huo
h)	<i>Nyumba *hilo</i>	Nyumba hiyo
i)	<i>Mipango *havo</i>	Mipango hiyo

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Jedwali Na. 6.1 linaonesha kuwa wajifunzaji walifanya dosari kwa kutumia vionyeshi visivyo sahihi kurejelea nomino tofauti. Kwa mfano, katika Mfano (a), kionyeshi *huu* kilichotumiwa kuashiria nomino *insha* si sahihi. Badala yake, mjifunzaji angetumia *hii* na kutunga tungo sahihi *insha hii*. Katika Mfano (b), mjifunzaji alitumia kionyeshi kisicho sahihi *huu* badala ya *hiyo* kuashiria nomino *siku* katika njeo iliyopita. Aidha, katika Mfano (c), nomino *maswali* inaashiriwa kwa kutumia kionyeshi kisicho sahihi *huu* badala ya *hayo*. Vilevile, dosari za matumizi ya vionyeshi visivyo sahihi zinazidi kubainika katika Mfano (d) ambapo mjifunzaji alitumia kionyeshi *huo* kimakosa badala ya *hiyo* kuashiria nomino karatasi. Yaani, mjifunzaji alitunga tungo isiyo sahihi *karatasi huo* badala ya *karatasi hiyo*.

Hali kadhalika, katika Mfano (e), kionyeshi *hiyo* kilichotumiwa kuashiria wakati si sahihi. Kionyeshi sahihi kilichopaswa kutumiwa ni *huo*. Katika Mfano (f), nomino *daktari* ingeashiriwa kwa kutumia kionyeshi *huyo* na wala si *huo*. Katika Mfano (g), nomino *muda* ingeashiriwa kwa kutumia kionyeshi *huo* badala ya *hii*.

Vilevile, katika Mfano (h), mjifunzaji alifanya dosari kwa kutumia kionyeshi kisicho sahihi *hilo* kurejelea nomino *nyumba* badala ya kionyeshi sahihi


hiyo. Sambamba na hilo, Mfano (i) pia unaonesha dosari ya matumizi ya kionyeshi kisicho sahihi *hayo* badala ya *hiyo*, kuashiria nomino *mipango*.

Matokeo ya uchanganuzi wa data katika kipengele hiki yanadhihirisha kufanyika kwa dosari mbalimbali za kimofosintaksia za matumizi yasiyo sahihi ya vionyeshi nya nomino za ngeli tofauti. Kwa mujibu wa matokeo haya, wajifunzaji wanakosea kanuni za matumizi ya kipengele hiki cha kisarufi kwa kushindwa kutambua vionyeshi sahihi nya nomino husika katika tungo wanazozitunga. Hali hii inaenda sambamba na mawazo ya Corder (1967) yanayojenga msingi mkuu wa Nadharia ya Usasanyuzi Dosari kwamba, dosari zinazofanywa na wajifunzaji lugha hutokana na wajifunzaji wenyewe kukosea kanuni za lugha lengwa.

4.6.2 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vivumishi nya Sifa

Kwa mujibu wa data za utafiti huu, katika matumizi ya vivumishi nya sifa, wajifunzaji walifanya dosari kwa kushindwa kutumia kiambishi sahihi cha nomino kwenye mzizi wa kivumishi. Mifano ya data zenye dosari za aina hii ni Insha Na. 4.6.2.

Insha Na. 4.6.2



Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Dosari zinazojitokeza katika insha hii zimeoneshwu kwa muhtasari katika Jedwali Na. 6.2.

Jedwali Na. 6.2: Vivumishi nya Sifa visivyo Sahihi

Na.	Dosari	Kwa Kiswahili Sanifu
a)	<i>Kila kitu ilikuwa *nzuri</i>	Kila kitu kilikuwa <u>kizuri</u>
b)	<i>Kazi *mzuri</i>	Kazi <u>nzuri</u>
c)	<i>Chakula *nzuri</i>	Chakula <u>kizuri</u>
d)	<i>Amekuwa mtu *nzima</i>	Amekuwa mtu <u>mzima</u>
e)	<i>Nyumba *warefu</i>	Nyumba <u>ndefu/majengo marefu</u>
f)	<i>Mavazi *nzuri</i>	Mavazi <u>mazuri</u>
g)	<i>Viato nzuri nya rangi jeusi</i>	Viato <u>vizuri</u> nya rangi nyeusi
h)	<i>Kiswahili mzuri</i>	Kiswahili <u>kizuri</u>
i)	<i>Pahali *nkubwa</i>	Pahali <u>pakubwa</u>

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari-Machi, 2023)

Data katika Jedwali Na. 6.2 inabainisha wazi kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari kutoptana na matumizi yasiyo sahihi ya vivumishi visifa kutoptana na kutoptumia viambishi sahihi vya nomino inayovumishwa kwenye mzizi wa kisifa kinachotumika. Mathalani, katika Mfano (a), kuna matumizi ya kivumishi kisifa *nzuri* ambacho kilitumiwa kurejelea nomino *kitu*. Nomino hii ni ya ngeli ya KI-VI, na hivyo, kiambishi sahihi kilichopaswa kutumiwa ni {ki-} na wala si {n-}. Kwa hivyo, tungo sahihi iliopaswa kutungwa ni *kila kitu kilikuwa kizuri*.

Katika Mfano (b), mjifunzaji alitunga tungo isiyo sahihi *kazi mzuri* badala ya *kazi nzuri*. Hapa mjifunzaji alitumia kiambishi awali {m-} badala ya {n-} kwenye mzizi wa kisifa. Hali kadhalika, katika Mfano (c), kuna dosari ya matumizi ya kivumishi kisifa *nzuri* badala ya *kizuri* kurejelea nomino ya ngeli ya KI-VI. Pia, katika Mfano (d), katika tungo *amekuwa mtu nzima*, mjifunzaji ametumia kiambishi {n-} kurejelea nomino mtu ya A-WA kwa mzizi wa kivumishi kisifa *zima*. Badala yake, mjifunzaji angetumia {m-} na kutunga tungo sahihi *amekuwa mtu mzima*.

Sambamba na hayo, dosari za matumizi yasiyo sahihi ya vionyeshi zinabainika katika Mfano (e), ambapo kiambishi {wa-} kinapachikwa kimakosa katika mzizi wa kisifa *refu* kuelezea nomino *nyumba*. Mjifunzaji alipaswa kutumiwa {n-} na kusema *ndefu*, yaani, *nyumba ndefu*. Isitoshe, katika Mfano (f), tungo **Insha Na. 4.6.3**

mavazi nzuri, ina dosari ya matumizi ya kivumishi kisifa kisicho sahihi kutoptana na kutumiwa kiambishi {n-} kinachowekwa kwenye mzizi wa kivumishi. Kiambishi {n-} si sahihi kwa nomino *mavazi*. Kiambishi sahihi ambacho kilipaswa kutumiwa katika tungo hii ni {ma-}. Hivyo, tungo kamili ilitakiwa kuwa *mavazi mazuri*. Katika Mfano (g), kuna dosari ya kutumiwa kivumishi kisifa *nzuri* kisicho sahihi kwenye nomino *viatu* badala ya *vizuri*. Aidha, katika Mfano (i), nomino pahali imevumishwa kwa kutumiwa kivumishi *mkubwa* ambacho si sahihi. Kiambishi sahihi ambacho kilipaswa kutumiwa ni {pa-}. Hivyo, mjifunzaji badala ya kutumiwa {m-} angetumia {pa-} na kusema *pahali pakubwa*.

Kama ilivyo kwenye matokeo yaliyobainika katika vipengele vya awali vya sura hii, matokeo ya utafiti katika kipengele hiki yanaonesha pia kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari za kimofosintaksia kutoptana na kushindwa kutumiwa kwa usahihi vivumishi visifa vya nomino za ngeli tofauti.

4.6.3 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vivumishi Vimilikishi

Kwa mujibu wa data za utafiti huu zilizokusanywa kutoptana na uandishi wa insha, usaili na ushuhudiaji, wajifunzaji walifanya dosari kutoptana na matumizi ya vimilikishi visivyo sahihi. Mifano ya tungo zenye dosari za aina hii inabainika katika Insha Na. 4.6.3 na Dondoo Na. 4.6.3.

SIKU YANGU YA KUANZA KUENDA MJINI LA KAMPALA

Mpongo

Kutembeteza dada yangu
Kutembeza la muusiko wa darasa la zaka

Kahka linizoni la muusiko wa darasa la zaka, ilianwa siku
miao la Juma mne, nitiamka mapenzi azubiki, nitianwa mocho wangu
na muuti ucungi wote.

He siku niti toka kuenda ni baba yangu Kutembeteza
dada yangu impendua fano kura mjni, la Kampala.

Tulipata motokaa yeti, tuliendo barabarani sana kabisa
kutembeteza tulitokaa mlni mlelo la Altoro Kitagumenda, nitianwa
bambooza zuri sana, nyumba nienye sana na wafee sana.

Alitokaa tulipata chakula kiba jesa mne za asubiki, Baba
wangu atifaya na kutokaa chakula nzuri sana. Mimi nitigaze
Chakula mlongo kusamifano ugati, matukarageku kusamabuluk sida
Sildura nzuri, lakin baba wangu alisense kusamifa
Tulipata nzuri.

Banda ya kula, tulipata motokaa yeti ile mossa, tuliendo
kwa Mbarabarani la Masaka. Banda ya sana nane, tulifika
mjni Nitikana kuona la Kampala, tuliendo kwa pabali makwico,
sana la ndege zilizimmo ulithia Entebbe Air Port. Nili ora vinta
ryingine sana kutoka Pathaki ile.

Baba yangu impendua atipiga simu kwa dada wete
kutuona lacini dada wete akicerwa nyuma yeti haitumice,
sana lacini bawale, tuliamo dada wete impendua, sana, tulisakemba
yege, alisense kusambo tunde kwa nyumbani yake

Tuliendo na yege kwa nyumbani yake baada ya kufa
nyumbani yake atipota na ryakulu rizuri sana na vinywadi,
viziuri sana. Nitikula sana ryakulu ryingi, sana. Banda ya
saa kumi za jioni, muone mme wa dada yangu atikucie na
vinywadi, na ryakulu kusamifano mkate nyame.

Siku ilakisi tulindo nyumbani ya dada wangu. Tuliendo
nyumbani yege.

Nito Siku ile silihatalisatice daima sana.
Mweneno ni mia mbili;

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Dondoo Na. 4.6.3

Tamthilia ya *Mizigo* ni tamthilia inaongea juu ya bwana Wamala na familia *wake. Mke *yake anaitwa Tinka na watoto yao ni wawili Kaija na Nyakake. Katika kijiji yao, ilikuwa ujisadi ambayo inaleta Wamala kukuwa masikini. Kazi yake ilikuwa kunywa pombe na kuja usiku *nyumba yake na makelele yake mingi kwa Tinka. Tinka anabeba mizigo yote ya familia na kujali mume na *watoto yao* kwa kuuza pombe ya Enguli na kupata pesa.

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Data katika Insha Na. 4.6.3 na Dondoo Na. 4.6.4 zinaonesha mifano ya tungo zenyé dosari za kimofosintaksia zilizofanywa na wajifunzaji kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya vivumishi vimilikishi. Mifano ya dosari hizo imeoneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 6.3.

Jedwali Na. 6.3: Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vimilikish

	Dosari	Kwa Kiswahili Sanifu
a	<u>Dada *wangu</u>	Dada <u>yangu</u>
b	<u>baba *wangu</u>	Baba <u>yangu</u>
c	<u>Motoka *yetu</u>	Gari letu
d	<u>Dada *wetu</u>	Dada <u>yetu</u>
e	<u>Nyumbani yake</u>	Nyumbani <u>kwake</u>
f	<u>Nyumbani *yetu</u>	Nyumbani <u>kwetu</u>
g	<u>Wamala na familia *wake</u>	Wamala na familia <u>yake</u>
h	<u>Mke *yake anaitwa</u>	Mke <u>wake</u> anaitwa
i	<u>Katika kijiji *yao</u>	Katika kijiji chao

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Jedwali Na. 6.3 linaonesha tungo zinazobainisha mifano ya dosari za matumizi ya vimilikishi visivyo sahihi. Dosari hizo zinafafanuliwa zaidi katika aya zinazofuata.

Katika mifano (a) na (b), kuna matumizi yasiyo sahihi ya kimilikishi “-angu”. Katika sarufi ya Kiswahili, majina ya ukoo hurejelewa kwa kutumia kimilikishi cha nafsi ya kwanza *yangu* katika umoja na *zangu* katika wingi. Hivyo, katika Mfano (a), wajifunzaji walitakiwa

kusema *dada yangu* na wala si *dada wangu*. Aidha, katika Mfano (c), tungo *motoka yetu* si sahihi katika Kiswahili. Katika Mfano (d), tungo *dada wetu* si sahihi kutokana na matumizi ya kimilikishi *wetu* badala ya *yetu*.


Aidha, kunabainika dosari za matumizi yasiyo sahihi ya kivumishi kimilikishi –ake. Kwa mfano, katika Mfano (e) kuna matumizi ya kimilikishi *yake* badala ya *kwake*, na vilevile, katika Mfano (f), kuna matumizi ya kimilikishi kisicho sahihi *wake* katika kirai *Wamala na familia wake*, badala ya *Wamala na familia yake*. Kadhalika, kuhusu matumizi ya kimilikishi –ake, katika Mfano (h), tungo *mke yake* si sahihi kutokana na matumizi ya kimilikishi yake badala ya *wake*, yaani, *mke wake*.

Mbali na hayo, matumizi ya kimilikishi –ao pia yalibainisha ufanyaji dosari miongoni mwa wajifunzaji. Kwa mfano, katika Mfano (i), kimilikishi *yao* kilichotumiwa kurejelea *kijiji* si sahihi. Badala yake, kimilikishi *chao* kingetumiwa na kuifanya tungo kuwa *katika kijiji chao*.

4.6.4 Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vivumishi vya Idadi

Data za utafiti huu zinaonesha kwamba wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda walifanya dosari kwa kushindwa kutumia vipatanishi sahihi vyा nomino kwa vivumishi viidadi katika tungo walizozitunga katika Kiswahili. Mifano ya tungo zenye dosari za aina hii inabainika katika Insha Na. 4.6.4.

Insha Na. 4.6.4



Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Data hii inadhihirisha kufanyika kwa dosari mbalimbali kuhusu matumizi ya kivumishi kiidadi.

Mifano ya dosari za aina hii imebainishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 6.4.

Jedwali Na. 6.4: Matumizi Yasiyo Sahihi ya Vivumishi vya Idadi

Na.	Dosari	Katika Kiswahili Sanfu
a)	<u>Rafiki yetu *moja</u>	Rafiki yetu <u>mmoja</u>
b)	<u>Tulikuwa watu *wingi</u>	Tulikuwa watu <u>wengi</u>
c)	<u>Mzee *moja</u>	Mzee <u>mmoja</u>
d)	<u>Miaka *mbili</u>	Miaka <u>miwili</u>
e)	<u>Mwanafunzi *moja</u>	Mwanafunzi <u>mmoja</u>
f)	<u>Miaka *tano</u>	Miaka <u>mitano</u>
g)	<u>Watu *vote</u>	Watu <u>wote</u>
h)	<u>Watu wingine wingi</u>	Watu <u>wengine wengi</u>
i)	<u>Watu *vote akuna ata *moja</u>	Watu <u>wote hakuna hata mmoja</u>
j)	<u>Vitu mengi</u>	Vitu <u>vingi</u>

Chanzo: Data Kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Jedwali Na. 6.4 linaonesha kuwa wajifunzaji walifanya dosari kwa kushindwa kutumia vivumishi sahihi vya idadi kulingana na nomino husika. Dosari hiso

zilionesha matumizi yasiyo sahihi ya viidadi viliviyolenga kutaja idadi mahususi ya nomino husika. Kwa mfano, katika mifano (a), (c) na (e), nomino

zinazorejelewa ni za ngeli ya A-WA, yaani, rafiki, mzee na mwanafunzi. Viambishi vyatengenezwa na ngeli hii ni {m-} na {wa} katika umoja na wingi, Hivyo, kiidadi sahihi ambacho kingetumiwa ni mmoja, yaani, *rafiki mmoja, mzee mmoja na mwanafunzi mmoja*. Sambamba na hili, katika Mfano (b), kiidadi *wengi* kilipaswa kutumiwa badala ya *wingi* kwenye nomino *watu*.

Aidha, katika Mfano (d), kiidadi *mbili* si sahihi. Kiidadi kilichopaswa kutumiwa ni *miwili*, yaani, miaka miwili. Pia, katika Mfano (f), kuna matumizi ya kiidadi kisicho sahihi, yaani, *tano* badala na *mitano*. Isitoshe, katika Mfano (g), njifunzaji alitunga tungo zenyetengeneza kwa kutumia kiidadi *yote* badala ya *wote*. Katika Mfano (h), kiidadi *mengi* si sahihi. Badala yake, tungo hiyo ilipaswa kuwa *vitu vingi*. Kadhalika, katika Mfano (i), kiidadi *yote* kwenye nomino *watu* si sahihi. Kiidadi sahihi ni *wote*. Vilevile, katika tungo (e), nomino *vitu* ingeambatana na kiidadi *vingi* badala ya mengi.

Matokeo haya kwa ujumla yamedhihirisha kuwa, wajifunzaji katika eneo tajwa wanafanya dosari za kimofosintaksia kutohukana na matumizi yasiyo sahihi ya vivumishi. Kahigi (2005 na 2008) anaeleza kuwa upatanishi wa kisarufi ni kipengele muhimu katika lugha yoyote na ni muhimu kuzingatia uambishi wa kivumishi kwa sababu utatizikaji katika lugha nyingi hutokana na kivumishi. Mawazo haya yanashadidia matokeo ya utafiti huu ambayo yanadhihirisha kutatizika kwa wajifunzaji katika uambishishaji wa vivumishi. Wesana-Chomi (2013) anakibainisha kivumishi kama kipashio kikuu cha kimofosintaksia. Anasema kwamba kivumishi ni kipashio cha kisintaksia pale ambapo kinatawala upatanisho wa kisarufi katika sentensi. Anasema kuwa, kisintaksia vivumishi vinajumuisha maneno ambayo yanaelezea nomino. Wesana-Chomi (keshatajwa) anaendelea kueleza kuwa, nomino lazima iakisi muundo wa vivumishi, vinginevyo, tungo itakayotoka haitakuwa sahihi kisarufi. Anasema kuwa, uzingativu wa viambishi vipatanishi huunda msingi wa upatanishi wa kisarufi na vinavyotakiwa kuzingatiwa.

Kwa mantiki ya maelezo ya wataalamu hawa, matumizi ya vivumishi katika lugha ya Kiswahili yana kanuni zake maalumu ambazo ni sharti zizingatiwe ili kuleta upatanisho mzuri katika sentensi. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, ni dhahiri kuwa wajifunzaji

walikosea kanuni za matumizi ya vivumishi vya Kiswahili, hivyo, kufanya dosari za kimofosintaksia. Hali hii inaafikiana na mawazo ya Corder (1967) katika NUD kwamba, dosari zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha hutokana na wajifunzaji wenye kukoza kanuni za lugha wanayo jifunza.

4.7 Matumizi ya Miundo ya Sentensi Isiyo Sahihi

Kwa mujibu wa data za utafiti huu, wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nichini Uganda pia hufanya dosari kwa kutozingatia miundo sahihi ya sentensi za Kiswahili sanifu katika ujifunzaji wao. Kutohukana na data zilizokusanywa kwa kutumia usaili na ushuhudiaji, dosari za miundo isiyo sahihi katika Kiswahili inabainika katika masimulizi ya wajifunzaji kama tunavyoweza kuona katika Dondoo Na. 4.7.1 na Dondoo Na. 4.7.1 kutohukana na masimulizi hayo ya wajifunzaji.

Dondoo Na. 4.7.1

Tulipanda basi ekatupeleka town ya Kampala. Mimi nachoka sana nasema rafiki wangu *tukeho anakataa. Yeye anasema mimi kwamba twende restaurant *tuleko chakula nakupata manyi ya kwenda *mugari ingine. Namsema kwamba nataka *twendeyo lakini ina fujo mingi. Mimi hapenda fujo sana. Tunaenda naona rafiki tulisoma yote *Ntare sekondari shule. Anapiga stori na sisi yote anafurahi...

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari-Machi, 2023)

Dondoo Na. 4.7.2

Mimi ukipigia kura, na kuwa kiongozi yenu zuri sana. Naleta umeme *mukijiji yote, watu yote anapata maji zuri *kunyumba yao. Tena mimi ukipa kura nakuwa mbunge, watoto yote *mukijiji wanaenda *mushule zuri mu primary na *mu sekondary. Pia ukinipa kura, nitakuenda kujenga hospitali nyingi ya wagonjwa ...

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Data katika madondoo Na. 4.7.1 na Na.4.7.2 zinadhihirisha dosari za matumizi ya miundo isiyo sahihi katika lugha ya Kiswahili. Mifano ya tungo zinazobainika katika madondoo haya imeoneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 7.

Jedwali Na. 7: Miundo Isiyo Sahihi katika Sentensi za Kiswahili

Na.	Dosari	Katika Kiswahili Sanifu
a)	<u>*Tukeko</u>	<u>Tukae kidogo</u>
b)	<u>*Tuleko</u>	<u>Tukale/tule kidogo</u>
c)	<u>Kwenda *mugari</u>	<u>Kwenda kwenye gari</u>
d)	<u>Nataka *twendeyo</u>	<u>Nilitaka twende huko</u>
e)	<u>Ntare *sekondari shule</u>	<u>Shule ya sekondari ya Ntare</u>
f)	<u>*mukijiji yote</u>	<u>Kijijini kote</u>
g)	<u>*kunyumba yao</u>	<u>Nyumbani kwao</u>
h)	<u>Mushule nzuri</u>	<u>Kwenye shule / katika shule nzuri</u>
i)	<u>Muprimay na Musekondary</u>	<u>Katika shule za msingi na sekondari</u>

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari-Machi, 2023)

Data katika Jedwali Na. 7 zinaonesha dosari zilizofanywa na wajifunzaji kutokana na matumizi ya miundo isiyokubalika katika sarufi ya Kiswahili. Dosari hizi zimeelezwu katika maelezo yanayofuata.

Katika mifano (a) na (b), tukichunguza tungo, *tukeko na tuleko* tunaona kwamba kuna matumizi ya mofu {-ko}. Kwa mujibu wa data za utafiti huu, ilibainika kuwa mofu hiyo hutumiwa katika lugha ya Kiganda ikiwa na maana ya kutenda jambo kwa kiasi fulani cha muda. Kwa maana hiyo, wajifunzaji waliiutumia wakidhani kuwa ni kielezi ambapo katika Kiswahili ni sawa na *tukae kidogo na tukale/tule kidogo*. Kwa hivyo, mifano hii inadhihirisha matumizi ya miundo isiyo sahihi katika tungo kama vile virai na sentensi za Kiswahili.

Aidha, katika Mfano (c), kwenye kirai *kwenda mugari*, katika neno gari kumepachikwa kiambishi awali {mu-}. Kwa mujibu wa data za utafiti huu, ilibainika kuwa mofu hiyo hutumiwa katika lugha za Kinyankole, Kikiga, Kinyoro, Kitoro na Kiganda, kwa maana ya *ndani au kwenye*. Hivyo, hapa mjifunzaji alikusudia kusema *kwenda ndani ya gari/ kwenda garini*.

Katika Mfano (d), tukichunguza tungo *nataka twendeyo*, tunaona kwamba mbali na mjifunzaji kutumia njeo ya wakati ujao badala ya wakati uliopita, ametumia pia muundo usio sahihi wa kirai kitenzi cha Kiswahili. Badala ya mjifunzaji kusema *twende huko alipachika {-yo}* katika neno twende kwa kudhani kuwa ni kioneshi. Hali kadhalika, katika mifano (f), (h) na (i), kuna matumiz ya {mu-} ambayo inapachikwa katika nomino *kijiji, shule*, na *Primary*. Kwa maana ya *kijiji, shulen* na *katika shule za msingi*.

Kwa ujumla, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba wajifunzaji wa Kiswahili katika shule nchini Uganda wanafanya dosari za kimofosintaksia kutokana na matumizi ya miundo isiyo sahihi katika sarufi ya Kiswahili. Inadhidihirika kuwa wajifunzaji wanakosea kanuni za miundo sahihi ya tungo za Kiswahili. Hali ambayo imedhihirishwa na matumizi

ya miundo ya lugha nyingine ambazo wanazifahamu. Ama kwa hakika, mawazo ya Corder (1964) kuwa wajifunzaji katika ujifunzaji lugha hufanya dosari kutokana na wenyewe kukosea kanuni, yanathibika kuwa kweli kutokana na matokeo ya utafiti huu. Yaani, wajifunzaji walikosea kuzingatia kanuni za miundo ya virai na sentensi za Kiswahili na kutumia miundo ambayo wameizoea katika lugha zao za kwanza, na hivyo, kufanya dosari za kimofosintaksia katika ujifunzaji wao.

4.8. Matumizi Yasiyo Sahihi ya Ukanushi

Matini andishi na simulizi za wajifunzaji zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha na ushuhudiaji pia zinadhihirisha kuwa wajifunzaji walifanya dosari za kimofosintaksia kwa kushindwa kukanusha tungo husika kwa usahihi. Mifano ya dosari za aina hii inabainika katika madondoo na insha ambazo zimesharejelewa katika vipengele vya awali vya sura hii. Mifano ya dosari hizo imeoneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 4.8 baada ya kuwasilisha mfano wa data iliyokusanywa kutokana na ushuhudiaji na kujadiliwa kwa pamoja.

Dondoo Na. 4.8:

Siku nilienda kupata results yangu ya UNEB mimi nilifurahi sana. Wazazi yangu *hapana kujuua mimi nitapita katika mitihani. Na mimi pia *sinajua mimi mwenyewe kama nafafulu mitihani kwa kuwa inakuwa ngumu sana. Shida mimi nilikata tamaa. Hakuna mtu anajua kama mitihani inarudi. Watu walikusemasema maneno kwa kushule yetu kuiba mitihani lakini sisi *hapana kuiba mitiani. Results ilikuja nimefurahi sana kabisa...

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari- Machi, 2023)

Dondoo Na. 4.8 linabainisha mifano ya tungo zenye dosari zilizofanywa na wajifunzaji kutokana na kushindwa kukanusha kwa usahihi. Jedwali Na. 8 linatoa muhtasari wa baadhi ya matokeo ya utafiti.

Jedwali Na. 8: Matumizi Yasiyo Sahihi ya Ukanushi

Na.	Dosari	Katika Kiswahili Sanifu
a)	<u>Siku ambayo *utaisahu</u>	Siku ambayo <u>sitaisahau</u>
b)	<u>Wazazi wangu *hapana juu</u>	Wazazi wangu <u>hawakujua</u>
c)	<u>Mimi *panaelewa</u>	Nilikuwa <u>sielewe</u>
d)	<u>Mama alikuwa *bado kwenda</u>	Mama alikuwa <u>hajaenda</u>
e)	<u>Nilisema *sinajua</u>	Nilisema <u>sijui</u>
f)	<u>Nilikuwa *sinajua</u>	Sikujuua
g)	<u>Walikuwa *wasipiti mitihani</u>	Walikuwa <u>hawapiti</u>
h)	<u>*Akuna aliyebak</u>	Hakuna aliyebak
i)	<u>Wazazi yangu *hapanakujuua</u>	Wazazi wangu <u>hawakujua</u>
j)	<u>Na mimi pia *sinajua</u>	Na mimi pia <u>sikujuua</u>
k)	<u>Sisi *hapana kuiba mitihani</u>	Sisi hatukuiba <u>mitihani</u>

Chanzo: Data kutoka Uwandani (Februari –Machi, 2023)

Mifano ya data zinazobainishwa katika Jedwali Na. 8 ni dosari zilizofanywa na wajifunzaji kwa kutumia ukanushi usio sahihi. Dosari hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:

Katika Mfano (a), kuna dosari ya kutumia {u-} badala ya mofu ya ukanushi {si}. Hii ilijitokeza katika insha nyingi zilizotungwa na wajifunzaji kutokana na zoezi walilopewa wajifunzaji: *Tunga insha yenyen urefu wa maneno yasiyoyozidi 300 juu ya siku amboyu hutaisahau daima*. Katika kuunda kichwa cha insha, wajifunzaji walitatizika sana kutumia ukanushi. Baadhi ya wajifunzaji walitunga tungo *siku utasahau* badala ya *siku amboyu sitaisahau*. Dosari kama hizi zilitokana na wajifunzaji kutobaini mofu za ukanushi wa nafsi ya kwanza katika umoja, yaani, *ni* na wakaishia kutumia mofu nyinginezo zisizokuwa sahihi na kufanya tungo nzima kutokuwa sahihi.

Aidha, kulibainika matumizi ya *pana/hapana* kama mofu ya ukanushi katika tungo za wajifunzaji. Mathalani, katika mifano (b), (c), (i) na (k), wajifunzaji walitumia mofu hii kwa maana na kinyume cha kufanya kwa tendo husika.

Kwa mfano, katika Mfano (b), mjifunzaji alisema *wazazi wangu hapana jua* badala ya *wazazi wangu hawakujua*. Katika Mfano (c), kuna tungo *mimi hapana elewa* badala ya *sikuelewa*. Mfano mwagine wa dosari kama hii ni katika (k) ambapo mjifunzaji alisema *sisi hapana kuiba mitihani* badala ya *sisi hatukuiba mitihani*.

Mbali na hayo, ilibainika kuwa wajifunzaji walishindwa kutumia hali ya ukanushi ya sentensi za njeo iliyopo. Dosari hii inabainika katika Mfano (e) na (f) katika sentensi *nilisema sinajua* na *nilikuwa sinajua*. Katika sentensi hizo, mjifunzaji alishindwa kutumia ukanushi sahihi kuonesha hali ya kutojua. Alisema *sinajua* badala ya *sijui*, na kutunga sentensi sahihi *nilisema sijui na sikuwa najua*. Hali kadhalika, mionganoni mwa dosari za ukanushi pia ilikuwamo matumizi ya *bado* kukanusha kauli husika. Kwa mfano, katika Mfano (d), mjifunzaji alisema, *mama alikuwabado kwenda*. Kwa maana ya, *mama alikuwa hajaenda*.

Fauka ya hayo, ilibainika pia kuwa wajifunzaji walifanya dosari za ukanushi kutokana na matumizi ya mofu {a} badala ya {ha} ya ukanushi wa nafsi ya tatu umoja. Kutokana na data zilizokusanywa kwa kutumia uandishi wa insha, inabainika kuwa wajifunzaji walifanya dosari za aina hii kutokana na tungo kama vile: *akuna mtu alibaki nyumbani* badala ya *hakuna mtu aliyebakini nyumbani*. Matumizi ya mofu {a-} badala ya {ha-} yalisababisha tungo kutokuwa sahihi kimofosintaksia kwa kuufanya utungo mzima kukosa maana.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari

nchini Uganda hufanya dosari za matumizi ya ukanushi usio sahihi. Dosari hizo zilibainika kutokana na tungo zilizotungwa na wajifunzaji ambazo zimethibitisha kutozingatia kanuni za ukanushi kwa usahihi na kutobaini na kutumia mofu za ukanushi kulingana na nomino husika, kitende na muktadha wa wakati, yaani njeo. Matokeo haya kwa hakika yanathibitisha ukweli wa mawazo ya Corder (1967) yanayoujenga mhimili wa Nadharia ya Usasanyuzi Dosari ambao husema kwamba, dosari katika ujifunzaji lugha hutokea kutokana na wajifunzaji wa lugha hiyo kukosea kanuni husika kutokana na kutozifahamu.

5.0 HITIMISHO

Makala haya yalilenga kubainisha dosari mbalimbali za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda. Data za utafiti zilipatikana kutoka uwandani kwa kutumia uchanganuzi matini na ushuhudiaji. Uchambuzi wa data uliongozwa na NUD iliyosisiwa na Corder (1967). Matokeo ya uchambuzi wa data yamedhihirisha kuwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali za kimofosintaksia. Dosari hizo ni: matumizi yasiyo sahihi ya vipatanishi vya kisarufi vya nomino, matumizi ya viambishi vya nomino visivyo sahihi, matumizi yasiyo sahihi ya vielezi vya mahali, virejeshi Matumizi yasiyo sahihi ya njeo, vivumishi, miundo ya sentensi isiyo sahihi na matumizi yasiyo sahihi ya ukanushi. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini Uganda hufanya dosari mbalimbali za kimofosintaksia katika ujifunzaji wao. Hivyo, makala haya yanatoa wito kwa walimu kumakinikia sana kipengele hiki katika ufundishaji ili kuwawezesha wajifunzaji kukuza kiwango chao cha umuduji na kujifunza Kiswahili kwa ufasaha.

MAREJELEO

- Corder, S. P. (1967). "The Significance of Learners' Errors". *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching*, 5, 161-170.
- Gawayise, A. (2016). *Ukakamaaji kwa Wajifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Jamii ya Wakinga*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Chepkwony, L. C. (2011). *Matatizo ya Kisarufi Mionganoni mwa Wanafunzi wa Kikipsigis Wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa Lugha Kadirifu*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Kahigi, K. K. (2005). "The sisumba Noun: Its Classes and Derivation". Katika Lot Publications. *Occasional Papers in Linguistics*, 1, 117-154.
- Kahigi, K. K. (2008). "Derivation in Sisumbwa". Katika Lot Publications. *Occassional papers in Linguistics*, 1, 117-154.
- Kisakwah, B. A. (2014). *Uchanganuzi wa Dosari na Muundo wa Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi*

- Sahili za Kiswahili Sanifu na za Kisuba.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Leijten, M na Van Waes, L. (2013). “Keystroke Logging in Writing Research Using Input log to Analyse na Visualize Writing Processes.” *Written Communication*, 30(3), 358-39.
 - Masereka, L. K (2021). *Athari za Kimofosintaksia za Kikonzo katika Ujifunzaji wa Kiswahili Ikiwa Lugha ya Pili Nchini Uganda.* Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
 - Mulei, M. (2023). *Uchunguzi wa Mofosintaksia ya Luganda katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu Wilayani Kampala, Uganda.* Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Maseno.
 - Mukuthuria, M. (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mifano kutoka kwa Wanafunzi wa Tigania, Kenya.* Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton.
 - Mutungu, B. N. (2001). *Dosari za Kileksia katika Insha na Chanzo Chake: Uchunguzi wa Shule Tano za Upili Wilayani Kiambu.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
 - Nyagah, S. K. (2016). *Uchunguzi wa Makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia Yanayojitokeza katika Kazi Andishi za Wanafunzi wa Shule za Sekondari Tigania Jimbo la Meru.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
 - Obara, J. M. (2014). *Uchunguzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
 - Ontieri, J. M. (2015). “Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kwanza katika Kiswahili: Mfano wa Lugha Teule za Kibantu Nchini Kenya”. *Mulika*, 34, 1-13.
 - Rapando, M. (2005). *Dosari za Kimofosintaksia katika Kazi za Kiswahili Zilizoandikwa na Wanafunzi wa Shule za Sekondari Jijini Nairobi.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
 - Ruragwerela, D. (2020). “Mikakati ya Kukabiliana na Dosari katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili Mionganoni mwa Wanafunzi wa Jamilugha ya Wahaya”. *Mkwawa Journal of Education and Development*, 4(2), 1-22.
 - Rutagwerela, D. (2022). Dosari za Kisarufi katika Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya pili Mionganoni mwa Wanafunzi wa Jamii Lugha ya Wahaya. Tasnifu ya Uzamivu (Hijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
 - Vincent, S. (2019). *Dosari za Kimofosintaksia Zifanywazo na Wajifunzaji wa Lugha ya Kiswahili wa Jamii Lugha ya Wairaki.* Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
 - Vincent, S. (2020). “Tathmini ya Dosari Zifanywazo na Jamii ya Wairaki katika Ujifunzaji wa Kiswahili”. *Kioo cha Lugha*, 18, 36-56.
 - Weigle, S. (1999). “Investigating Rate/Prompt Interactions in Writing Assessment: Quantitative and Qualitative Approaches”. *Assessing Writing*, 6(2), 145-178.

Cite This Article: Anifah Atuhaire & Adventina Buberwa (2025). Dosari za Kimofosintaksia Zinazofanywa na Wajifunzaji wa Kiswahili katika Shule za Sekondari Nchini Uganda. *East African Scholars J Edu Humanit Lit*, 8(5), 139-157.
